**East African Journal of Swahili Studies**
eajss.eanso.org
**Volume 6, Issue 1, 2023**
**Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475**
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Matumizi ya Kiswahili katika Mawasiliano na Uongozi wa Kidini katika Shule za Upili Nchini Kenya: Mfano wa Shule ya Wasichana ya Itigo

*Joachim Kipchirchir Melly[1*] na Prof. Ernest Sangai Mohochi, PhD[1]*

[1] Chuo Kikuu cha Kibabii, S. L. P. 1699 -50200, Bungoma – Kenya.
[*] Barua pepe ya mawasiliano: mellyjoachim@gmail.com

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1422**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*11 Septemba 2023*

**Istilahi Muhimu**:

*Mawasiliano, Dini, Kiswahili, Uongozi.*

**IKISIRI**

Utafiti huu ulichunguza matumizi ya Kiswahili katika mawasiliano na uongozi wa kidini katika shule ya wasichana ya Itigo. Ulilenga kubaini jinsi lugha ya Kiswahili hutumika katika kuwasilisha maudhui ya kidini, sera za matumizi ya lugha, na athari ya matumizi ya lugha ya Kiswahili katika kuwasilisha ujumbe wa kidini. Nadharia ya umilisi mawasiliano yake Dell Hymes (1966) iliongoza utafiti. Data ilikusanywa kwa kutumia hojaji, mahojiano na uchunzaji. Wanafunzi thelathini wa kidato cha nne, viongozi kumi wa kidini wa wanafunzi na kasisi mmoja wa shule walihusishwa katika ukusanyaji wa data. Matokeo yalibaini kuwa sera ya lugha katika shule ya wasichana ya Itigo ilipendelea matumizi ya Kingereza kama lugha ya mawasiliano. Wanafunzi walisema kuwa lugha ya Kiswahili inapotumika katika mahubiri, ujumbe hueleweka zaidi. Vilevile, ilidhihirika kuwa viongozi wa kidini wa wanafunzi hutumia lugha ya Kiswahili kuwasiliana katika mikutano yao lakini wao huandika kumbukumbu kwa lugha ya Kiingereza. Isitoshe, ilibainika kuwa lugha anayoitumia zaidi kasisi wa shule katika mahubiri yake ni Kiingereza. Licha ya uwezo wa Kiswahili katika kufanikisha mawasiliano kuhusu maswala ya kidini shuleni, Kiingereza ndicho hutumika zaidi. Kunahitajika mabadiliko katika sera ya lugha shuleni ili kuipa lugha ya Kiswahili nafasi zaidi katika mawasiliano ya kidini.

**APA CITATION**

Melly, J. K., & Mohochi, E. S. (2023). Matumizi ya Kiswahili katika Mawasiliano na Uongozi wa Kidini katika Shule za Upili Nchini Kenya: Mfano wa Shule ya Wasichana ya Itigo *East African Journal of Swahili Studies*, *6*(1), 339-349. https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1422.

**CHICAGO CITATION**

Melly, Joachim Kipchirchir and Ernest Sangai Mohochi. 2023. "Matumizi ya Kiswahili katika Mawasiliano na Uongozi wa Kidini katika Shule za Upili Nchini Kenya: Mfano wa Shule ya Wasichana ya Itigo". *East African Journal of Swahili Studies* 6 (1), 339-349. https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1422.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1422

**HARVARD CITATION**

Melly, J. K., & Mohochi, E. S. (2023) "Matumizi ya Kiswahili katika Mawasiliano na Uongozi wa Kidini katika Shule za Upili Nchini Kenya: Mfano wa Shule ya Wasichana ya Itigo", *East African Journal of Swahili Studies*, 6(1), pp. 339-349. doi: 10.37284/jammk.6.1.1422.

**IEEE CITATION**

J. K., Melly, & E. S., Mohochi "Matumizi ya Kiswahili katika Mawasiliano na Uongozi wa Kidini katika Shule za Upili Nchini Kenya: Mfano wa Shule ya Wasichana ya Itigo", *EAJSS*, vol. 6, no. 1, pp. 339-349, Sep. 2023.

**MLA CITATION**

Melly, Joachim Kipchirchir & Ernest Sangai Mohochi. "Matumizi ya Kiswahili katika Mawasiliano na Uongozi wa Kidini katika Shule za Upili Nchini Kenya: Mfano wa Shule ya Wasichana ya Itigo". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 6, no. 1, Sep. 2023, pp. 339-349, doi:10.37284/jammk.6.1.1422.

## UTANGULIZI

Madhumuni ya utafiti huu ni kuchunguza matumizi ya Kiswahili katika mawasiliano na uongozi wa kidini katika shule za upili. Katika kuchunguza matumizi ya Kiswahili, utafiti utachukua shule ya wasichana ya Itigo kama mfano. Misiko (2008) anahoji kuwa lugha ni muhimu katika mawasiliano ya binadamu kwani ni chombo cha kupashana habari na kuwasiliana. Matokeo ya kuwasiliana huku ni kuafikiana na kufarakana; kujenga na kubomoa. Matokeo haya hutegemea taarifa zinazotolewa, na namna zinavyowasilishwa. Kwa hivyo ni lazima taarifa zinazotolewa zitolewe kwa njia faafu na kwa lugha inayoeleweka. Davis (1976) anaeleza kuwa, mawasiliano ni upitishaji wa habari na maelewano kutoka kwa mtu mmoja hadi kwa mwingine. Anafafanua kuwa mawasiliano ni mfumo wa usafirishaji wa ujumbe kutoka kwa mtuma ujumbe hadi kwa mpokea ujumbe kwa kutumia nyenzo kama vile lugha.

Misiko (2008) anaendelea kueleza kuwa lugha ya Kiswahili imekua na kuenea kimatumizi kutokana na jitihada za wakereketwa wake. Ndiyo lugha inayotumika sana nchini Kenya katika mawasiliano. Kwa mujibu wa katiba ya Kenya (2010), Kiswahili ni lugha ya kwanza rasmi na lugha ya taifa. Wananchi wengi wanaitumia lugha hii katika kufanikisha mawasiliano yao. Lugha ya Kiswahili vile vile inatumika shuleni kama lugha ya mawasiliano. Aidha, lugha hii inafundishwa kama somo la lazima katika shule za msingi na za upili. Kufundishwa kwake kunalenga kuwapa wanafunzi umilisi wa kuizungumza kwa ufasaha. Wanastahili kuhamisha mafunzo ya darasani hadi katika hali halisi ya mazungumzo. Kwa hivyo inatarajiwa kuwa wanafunzi katika shule za upili wanazungumza kwa kufuata kanuni za sarufi. Hali hii itafanikisha mawasiliano kwa kutumia Kiswahili shuleni.

Dini ni muhimu sana katika maisha ya binadamu na katika mazingira ya shule za upili. Kando na kupewa mafunzo ya darasani, wanafunzi wanastahili kupewa fursa ya kupata ujumbe wa kidini. Hali hii huwasaidia wanafunzi kulelewa katika msingi wa maisha ya imani, maadili na utu wema dhidi ya mmomonyoko wa kimaadili unaoendelea kuikumba jamii kwa kasi ya ajabu hasa kutokana na athari kubwa ya matumizi ya mitandao ya kijamii. Kwa hivyo wanafunzi wanapaswa kupata fursa ya kushiriki katika ibada. Wanafunzi wengi kwa sasa wanaiga mambo kutoka kwenye mitandao ya kijamii. Hali hii huenda ikawafanya kuchanganyikiwa kimaisha. Katika kuwasilisha ujumbe wa kidini, lugha inayotumika ni muhimu katika kuleta athari inayotarajiwa kwa wanafunzi. Hali hii inaafiki maelekezo ya nadharia ya umilisi mawasiliano yake Dell Hymes (1966) kwamba madhumuni makuu ya matumizi ya lugha ni kuwasiliana kwani lugha ni mfumo wa kueleza maana. Lugha zinazotumiwa shuleni ni Kiingereza na Kiswahili. Kwa hivyo inatarajiwa kwamba lugha hizi mbili zinatumiwa katika kuwasilisha ujumbe wa kidini kwa wanafunzi.

Shule ya wasichana ya Itigo ni shule ya mkoa inayopatikana katika kaunti ndogo ya Chesumei katika kaunti ya Nandi. Shule hii ilianzishwa mwaka wa elfu moja mia tisa themanini na saba (1987). Inafadhiliwa na kanisa la AIC. Mkuu wa shule ni

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1422

Daktari Juliah Samoei. Shule ya wasichana ya Itigo ina wanafunzi mia tisa na sabini na mmoja. Vile vile ina walimu arobaini na saba. Shule ya Wasichana ya Itigo ina idara nyingi. Idara hizi ni idara za kiakademia kama vile idara ya lugha na idara ya sayansi. Vile vile kuna idara zisizo za kiakademia kama vile idara za michezo, dini na ushauri na nasaha. Idara hizi ni muhimu sana katika kuwasaidia wanafunzi kuimarika katika nyanja zote. Idara ya dini inaongozwa na Kasisi wa shule. Kuna mwalimu anayesimamia idara hii. Isitoshe kuna kamati ya wanafunzi wanaopanga shughuli za kidini. Wanafunzi hupewa fursa ya kuomba Jumapili kama siku maalum ya maombi. Kando na hili wanashiriki ibada kila Jumatano asubuhi kuanzia saa moja unusu hadi saa mbili. Aidha, Alhamisi kuanzia saa kumi hadi saa kumi na moja jioni. Wanafunzi vile vile hupata fursa ya kufanya maombi kabla ya gwaride la Jumatatu na Ijumaa, na kasisi wa shule hupewa fursa kutoa ujumbe wa kidini kwa wanafunzi. Kutokana na hali hii ni dhahiri kuwa wanafunzi katika shule ya wasichana ya Itigo wanapata muda wa kutosha kushiriki katika maombi. Katika kufanikisha maombi na mahubiri haya, lugha lazima itumike katika mawasiliano. Dell Hymes (1966) katika nadharia yake ya umilisi mawasiliano anahoji kuwa lugha inayotumika katika mawasiliano ni lugha ambayo inaeleweka kwa watu wote. Inatarajiwa basi kuwa katika muktadha wa shule za upili, lugha zinazotumika ziwe zinazoeleweka kwa urahisi na wahusika wote.

## MATUMIZI YA KISWAHILI SHULENI

Bryman (2008) anasema kuwa lugha ya kufundishia ni lugha mahususi inayoteuliwa na taifa ili kutumika katika shughuli za kutoa elimu rasmi katika nchi. Baadhi ya nchi huwa na lugha zaidi ya moja za kufundishia. Kwa mfano Tanzania ambapo elimu ya shule za msingi na elimu ya watu wazima huendeshwa kwa lugha ya Kiswahili. Elimu ya sekondari na ya chuo kikuu hutolewa kwa Kiingereza. Hata hivyo, katika siku za hivi karibuni serikali ya Tanzania imekuwa katika harakati za kuwezesha matumizi ya Kiswahili kama lugha rasmi ya kufundishia katika ngazi zote za elimu nchini humo. Nchini Kenya na Uganda, lugha ya kufundishia ni Kiingereza kuanzia shule za chekechea hadi shule za upili isipokuwa katika baadhi ya masomo kama vile Kiswahili. Taifa la Rwanda nalo lilibadili lugha ya kufundishia kutoka Kifaransa hadi Kiingereza. Nchi nyingi za Ulaya hutumia lugha mame zao kama lugha za kufundishia.

Kulingana na Kipchirchir (2019) Kiswahili ni somo la lazima katika shule za msingi na upili. Hii ni kutokana na dhima na umuhimu wake nchini Kenya. Ni lugha rasmi na lugha ya taifa ambayo imetambulika kuwa na uwezo wa kuleta umoja wa kitaifa. Fauka ya haya, Kiswahili si lugha ya tabaka au kabila moja. Ni lugha ambayo watu wa kila kabila na rika katika taifa zima wanaweza wakadai kuwa ni yao. Kiswahili kinachangia katika ujenzi wa taifa. Taifa linahitaji maarifa ya kuchambua na kuelewa nyenzo za kudumisha jamii na kuyatawala mazingira. Lugha ya Kiswahili inafaa sana kupitishia maarifa, dhana na stadi hizi.

Misiko (2008) anahoji kuwa ni fahari kuu kuona kuwa Kiswahili ni lugha ya taifa la Kenya. Hali hii imeonyesha cheche za udhihirisho kuwa imesaidia sana katika kueneza maendeleo ya siasa, elimu, utamaduni na dini. Kwa kutumia Kiswahili, wanafunzi wanabadilishana mawazo. Jambo hili ni msingi wa mwingiliano mwema, uelewano na ushirikiano. Mafunzo ya lugha ya Kiswahili, hasa mitindo na sajili mbalimbali humwezesha mwanafunzi kufahamu kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili kutegemea miktadha, kaida na miiko katika jamii za kiafrika. Huu ndio msimamo wa nadharia ya mawasiliano yake Dell Hymes (1966) kwamba jukumu muhimu la ujifunzaji wa lugha ni mawasiliano yanayofaa katika muktadha maalum. Hili ni muhimu kwani imekadiriwa kuwa lugha ya Kiswahili inazungumzwa na mamilioni ya wakazi wa mataifa mbalimbali ya Afrika, licha ya mengine yaliyo nje ya bara Ia Afrika.

Kwa hivyo pana haja ya kutoa mafunzo kabambe yatákayomwezesha mwanafunzi kuwa na umilisi wa kutumia Kiswahili katika shughuli za kila siku. Jambo hili ni muhimu zaidi tukizingatia kuwa lugha

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1422

ya Kiswahili ni lugha ya pili kwa wengi wa wakenya. Halikadhalika, inakabiliwa na maingiliano ya lugha na vilugha vinginevyo. Kama lugha ya pili, inahitaji kutolewa mwongozo mzuri wa mafunzo. Wanafunzi wanapaswa kuhimizwa kutumia lugha ya Kiswahili katika mawasiliano yao shuleni ili kuafikia malengo haya. Nadharia ya umilisi wa mawasiliano ya Dell Hymes (1966) inasema kuwa mtu hujifunza lugha zaidi kwa kuitumia lugha hiyo. Kwa mujibu wa Misiko (2008), sera ya lugha ni utaratibu uliowekwa na serikali kuhusu matumizi ya lugha ambapo kuna lugha kadhaa na kila lugha ikapewa dhima zake ambazo inatarajiwa kutekeleza. Kwa kuwa Waingereza walikidharau Kiswahili, sera zao hazikuruhusu kitumiwe kama lugha ya kufundishia katika shule zaidi ya shule za msingi; badala yake Kiingereza kilitumika. Matumizi ya Kiswahili shuleni yalitokana na mkutano wa 1925 ambapo wakuu wa Elimu wa nchi zote za Afrika Mashariki walikutana kuzungumza kuhusu lugha moja ya wenyeji ambayo ingetumika kufundishia katika nchi zote nne za Afrika Mashariki (Massamba na Wenzake, 2001). Matokeo yalikuwa ni uteuzi wa lugha ya Kiswahili. Kutokana na uamuzi huo, pamoja na matumizi yake katika shughuli nyingi, Kiswahili kiliibuka kuwa *lingua franca* ya Afrika Mashariki iliyotumika kwingi. Lugha ya Kiswahili inatumika katika mawasiliano nchini Kenya kwa ujumla. Vilevile, inatumika kwa mawasiliano katika taasisi za elimu. Kwa hivyo, ilikuwa muhimu kuchunguza jinsi lugha hiyo inavyotumika katika mawasiliano ya shughuli za kidini katika shule ya wasichana ya Itigo.

Oduori (2002), anashadidia umuhimu wa kuwepo kwa mwelekeo imara wa matumizi ya Kiswahili kwa kudai kwamba lugha, hasa, inayotumiwa na kuwashirikisha watu wengi inaweza kuwa kifaa muhimu kwa maendeleo ya nchi. Maoni ya Oduori (2002) yanaafikiana na maelekezo ya nadharia ya umilisi mawasiliano yake Dell Hymes (1966) kwamba lugha inayoeleweka na watu wengi ni nyenzo muhimu katika kufanikisha mawasiliano. Kiswahili kinaeleweka kwa watu wengi nchini Kenya. Ni kwa msingi huu ndipo utafiti huu ulilenga kubaini jinsi lugha hiyo inaweza kuwashirikisha wanafunzi katika shughuli za kidini na kuwapa fursa ya kujiendeleza ipasavyo katika masuala ya imani.

Mbaabu (1978) anasema kwamba nchini Kenya Kiingereza ni lugha rasmi inayotumika katika shughuli nyingi za serikali ilhali Kiswahili ni lugha ya taifa. Misiko (2008), anasema kuwa Agosti 1969 Rais wa kwanza wa jamhuri ya Kenya hayati Jomo Kenyatta alisema kwamba Kiswahili kitumike katika bunge kwani ndiyo lugha ya wananchi. Alibashiri kwamba wakati utafika ambapo kila kitu kitafanyika kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Ubashiri huu uliongoza utafiti huu kubaini matumizi ya Kiswahili katika kufanikisha mawasiliano ya kidini katika shule ya wasichana ya Itigo.

Anavyosema Mbaabu (1978), nchi ambazo zimeamua kutumia lugha zao katika shughuli zote za kitaifa na ufundishaji hadi kiwango cha juu zimefanikiwa. Ametoa mfano wa nchi kama vile China na Vietnam Kaskazini. Kwa mujibu wa Misiko (2008), Vietnam Kaskazini ilijikomboa kutoka kwa koloni ya Ufaransa mwaka wa 1954. Miaka kumi baadaye (1964), ilichapisha vitabu vikiwemo vya Teknolojia hadi kiwango cha chuo kikuu katika lugha yao ya Kivietnam ilhali lugha yao ilikuwa imedidimizwa zaidi na Wafaransa na haikuwa na nafasi bora kama Kiswahili wakati wa utawala wa Waingereza. Kwa upande mwingine China hutumia Kichina katika shughuli zake zote ikiwemo biashara na lugha yake imekubalika kuwa mojawapo ya lugha zinazotumika katika mikutano ya Umoja wa Mataifa.

Kwa mujibu wa Osore (2001), Kiingereza ni lugha ya wenye uwezo ilhali Kiswahili ni lugha ya watu wa kawaida katika nchi zote za Afrika Mashariki. Anasema kwamba kwa vile ni mtu wa kawaida anayehitaji kupashwa habari kuhusu masuala ya maendeleo, lugha faafu ni Kiswahili ambacho ni nyenzo nzuri katika kuwasilisha maarifa muhimu. Hivi ndivyo asemavyo Dell Hymes (1966) kuwa lugha inayoeleweka na watu wengi ni nyenzo muhimu katika kufanikisha mawasiliano. Masuala ya kidini kwa wanafunzi ni muhimu sana ili kuwakuza kitabia kadri wanavyokua. Nini nafasi ya Kiswahili

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1422

katika kuwasilisha jumbe za kidini na hivyo kuthibitisha mawazo ya Osore (2001) kwamba Kiswahili ni nyenzo nzuri katika kuwasilisha maarifa muhimu kama vile masuala ya kidini kwa wanafunzi wa shule za upili?

Misiko (2008), akimnukuu Kabaji (2002), analalamika kwamba kucheleweshwa kwa Kiswahili kufanywa lugha ya lazima katika shule za msingi na sekondari na wataalamu wa elimu lilikuwa kosa kubwa. Hali hiyo imeighrarimu serikali kwani kuna kizazi cha Wakenya wa umri wa zaidi ya miaka thelathini ambao weledi wao katika Kiswahili si mzuri. Anasema kutokana na kuanzishwa kwa mfumo wa elimu wa 8-4-4, Wakenya wote waliokwenda shuleni wanaweza kusoma Kiswahili. Anazidi kudai kwamba Kiswahili kimeibuka kuwa lugha mama kwa Wakenya wengi wanaoishi mijini. Aidha, kutokana na watu wengi kutoka makabila mbali mbali kuhamia mijini, hali hiyo hulazimisha watoto wafundishwe kwa lugha ya Kiswahili. Hili linaipa lugha ya Kiswahili nafasi nzuri ya kutumika shuleni katika mawasiliano yote. Mawasiliano ya kidini kwa wanafunzi yanaweza kuleta manufaa iwapo lugha ya Kiswahili itatumika. Ndiposa utafiti ulilenga kuchunguza jinsi lugha ya Kiswahili hutumika katika kuwasilisha ujumbe wa kidini kwa wasichana wa shule ya Itigo.

## NAFASI YA KISWAHILI KATIKA MAWASILIANO YA KIDINI SHULENI

Oduori (2002), anafafanua kwamba, Kiswahili ni lugha inayopaswa kutumiwa katika nyanja zote za mawasiliano ya kitaifa hasa katika shule. Ni lugha inayofahamika vizuri kwa wanafunzi na walimu. Anaendelea kusisitiza kwamba nchi nyingi duniani ambazo hutumia lugha zake huonyesha mafanikio katika nyanja za uchumi, siasa na jamii. Dini, ni muhimu sana katika ustawi wa mwanafunzi na ni muhimu kutumiwa lugha inayoeleweka katika kuwasilisha maudhui ya kidini kwa wanafunzi wa shule za upili. Hili linaona na maoni ya Dell Hymes (1966) katika nadharia ya umilisi mawasiliano kuwa matamshi yanayoeleweka na watu wengi katika mazungumzo ndiyo lengo kuu la matumizi ya lugha. Taifa la Uchina ni mojawapo ya mataifa yanaoonyesha mfano mzuri wa kutumia lugha yake kufundishia watu wake na matokeo yake ni kuwa na maendeleo makubwa ya kiuchumi. Katika mantikiki hiyo, Kiswahili kinapaswa kutumiwa katika mawasiliano shuleni hasa mawasiliano ya kidini.

Suala la nidhamu limekuwa changamoto katika shule za upili. Visa vya uchomaji wa shule vimekithiri katika shule za upili. Hii inatokana na upotovu wa nidhamu baina ya wanafunzi hawa. Nyimbo za kizazi kipya nazo zimeshika kasi sana miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili. Baadhi ya nyimbo hizi zinaeneza tabia hasi kama vile matumizi ya mihadarati na ngono miongoni mwa vijana. Mafunzo ya kidini yanaweza kutumika katika kukashifu tabia hizi. Lugha ya Kiswahili inaweza kutumika katika kuwasilisha maudhui haya kwa kuwa ni lugha inayoeleweka baina ya wanafunzi wote. Ni katika msingi huu ndipo utafiti huu ulilenga kuchunguza matumizi ya Kiswahili katika kuwasilisha maudhui ya kidini katika shule ya wasichana ya Itigo. Utafiti huu ulilenga; Kuchunguza jinsi lugha ya Kiswahili inatumika katika kuwasilisha ujumbe wa kidini katika shule ya upili ya Itigo na kutathmini athari za matumizi ya lugha ya Kiswahili katika kuwasilisha ujumbe wa kidini katika shule hiyo.

## NADHARIA YA UTAFITI

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya umilisi mawasiliano yake Dell Hymes (1966) iliyo na mihimili ifuatayo;

- Maana ya miundo husisitizwa kwani lengo kubwa la nadharia hii ni mawasiliano. Madhumuni makuu ya lugha ni kuwasiliana kwani lugha ni mfumo wa kueleza maana.

- Vipashio muhimu vya lugha siyo vile vya kisarufi na kimuundo tu lakini pia vile vya kimawasiliano.

- Kanuni za kisarufi na mbinu nyinginezo zinatumiwa inapoonekana kuwa lazima.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1422

- Mtu hujifunza lugha zaidi kwa kuitumia.

- Jukumu muhimu la ujifunzaji wa lugha ni mawasiliano yanayofaa katika muktadha maalum.

- Lugha inayoeleweka na watu wengi ni nyenzo muhimu katika kufanikisha mawasiliano.

Nadharia ya umilisi mawasiliano ilifaa utafiti huu kwa kuwa iliongoza utafiti katika kuthibitisha kuwa madhumuni makuu ya matumizi ya lugha ni kuwasiliana. Vilevile ilidhihirika kuwa vipashio muhimu vya lugha siyo vile vya kisarufi na kimuundo tu lakini pia vile vya mawasiliano. Kwa hivyo katika kuwasilisha maudhui ya kidini, mawasiliano bora yalifaa zaidi wala si uzingatiaji wa kanuni za sarufi. Wanafunzi walikiri kuwa lugha ya Kiswahili inapotumika katika mahubiri ujumbe hueleweka zaidi. Kwa jumla, nadharia hii iliuongoza utafiti katika kudhihirisha kuwa cha muhimu ni mawasiliano bora na kwamba njia bora kwa wanafunzi kujifunza lugha ni kuitumia katika mawasiliano yao yote, ikiwa ni pamoja na matumizi yake katika maswala ya kidini. Kwa hivyo wanapaswa kuitumia lugha ya Kiswahili katika mawasiliano yao ya mara kwa mara ili waweze kuwa na umilisi ulio imara.

## MBINU ZA UTAFITI

Utafiti huu ulifanyika katika shule ya Wasichana ya Itigo. Shule hii inapatikana katika kaunti ndogo ya Chesumei iliyoko katika Kaunti ya Nandi, nchini Kenya. Shule ya wasichana ya Itigo ni mojawapo ya shule za mkoa katika kaunti ya Nandi. Shule hii iliteuliwa kwa kuwa ina sifa zote za shule za mkoa nchini Kenya kwa hivyo ni kiwakilishi kizuri cha shule hizi. Vilevile, iliteuliwa kwa kuwa inathamini na kuweka msingi imara katika masuala ya kidini. Aidha, lugha inayotumika mara nyingi katika mawasiliano yote siku ya Jumapili katika shule hiyo ni Kiswahili.

Kothari (2004), anasema kuwa usampulishaji ni mchakato wa kuteua sampuli kutoka katika kundi lengwa. Naye Sharman (1983), anasema kuwa sampuli ni sehemu ndogo ya vitu au watu wanaotafitiwa ili kudhihirisha sifa sawa za idadi kubwa ya vitu au watu inayowakilisha ili kupata matokeo yanayoweza kuaminika. Utafiti huu ulitumia usampulishaji wa kimakusudi unaoelezwa na Mugenda na Mugenda (1999) kama mbinu ambayo humwezesha mtafiti kuchukua data kutoka kwa watafitiwa kulingana na madhumuni ya utafiti wake. Utafiti huu ulimhusisha kasisi wa shule kwa kuwa ndiye mhusika mkuu katika masuala ya kidini katika shule ya Itigo. Viongozi kumi wa kidini wa wanafunzi vilevile walihusishwa kwa lengo la kuchunguza jinsi wanavyotumia lugha ya Kiswahili katika shughuli za kidini na mikutano yao. Wanafunzi thelathini wa kidato cha nne vile vile walihusishwa katika kujaza hojaji kwa kuchukua asilimia thelathini ya wanafunzi wote wa kidato cha nne. Wanafunzi wa kidato cha nne walihusishwa kwa kuwa wao wamekuwa katika shule hii kwa miaka minne na ilikisiwa kuwa wameshiriki ibada nyingi kuliko wenzao katika madarasa mengine.

Utafiti huu ulizingatia njia mbili katika kukusanya data; hojaji na uchunzaji. Kwa mujibu wa Kothari (1993), hojaji ni kifaa faafu cha kukusanyia data hasa katika tafiti zinazohusisha idadi kubwa ya watoa habari kwani ni rahisi kupata habari kwa muda mfupi. Anaeleza kuwa licha ya gharama ya chini hojaji hutoa muda wa kutosha kwa mhojiwa kutoa majibu anayoyafikiria. Mbinu hii ilifaa kwa kuwa iliwezesha ukusanyaji wa data kwa muda mfupi.

Kwa mujibu wa Onen (2005), uchunzaji ni ushuhudiaji wa tukio linapotendeka na kukusanya taarifa zake. Ni kitendo cha kuchunguza watafitiwa wanafanya nini badala ya kuwauliza maswali. Naye Kipchirchir (2019) anasema kuwa uchunzaji ni njia muhimu sana katika utafiti kwani ndiyo njia ya pekee isiyo na ubaguzi. Ni kwa msingi huu ndipo uchunzaji ulichaguliwa kukusanya data kuhusu jinsi lugha ya Kiswahili inatumika katika kuwasilisha ujumbe wa kidini katika shule ya wasichana ya Itigo. Katika uchunzaji huu taarifa kuhusu jinsi lugha ya Kiswahili inavyotumika katika ibada za wanafunzi ilikusanywa kwa kushiriki ibada hizo.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1422

**MATUMIZI YA KISWAHILI KATIKA MAWASILIANO NA UONGOZI WA KIDINI**

Sehemuu hii ya makala inawasilisha matokeo ya utafiti huu ili kuonyesha hali halisi katika shule ya upili ya wasichana ya Itigo. Matokeo yamejadiliwa kwa kuzingatia majibu yaliyotolewa kwa maswali ya hojaji, maswali ya mahojiano na mwongozo wa uchunzaji.

**Sera ya Lugha**

Miongoni mwa maswala muhimu yaliyohakikiwa ni sera ya lugha katika shule ya wasichana ya Itigo. Matokeo ni kama yanavyodhihirika katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali 1: Sera ya Lugha katika Shule ya Itigo**

| Matumizi ya Lugha | Idadi ya majibu | Asilimia % |
|---|---|---|
| Kiswahili kimepuuzwa | 13 | 43% |
| Kiswahili kimepewa kipaumbele | 1 | 4% |
| Kiingereza kimepewa kipaumbele | 12 | 40% |
| Kiswahili hakijapewa nafasi sawa na Kiingereza | 4 | 13% |
| **Jumla** | **30** | **100%** |

Kutokana na matokeo katika *Jedwali 1*, asilimia 43 (N=13) ya wanafunzi thelathini waliohojiwa walikubali kuwa sera ya lugha katika shule ya wasichana ya Itigo imepuuza Kiswahili. Nayo asilimia 4 (N=1) ya wanafunzi thelathini waliohojiwa ilikiri kwamba Kiswahili kimepewa kipaumbele katika utekelezaji wa sera ya lugha katika shule ya wasichana ya Itigo. Isitoshe asilimia 40 (N=12) ilikubali kuwa Kiingereza kimepewa kipaumbele katika sera ya lugha shuleni. Hatimaye asilimia 4 (N=13) ilithibitisha kuwa Kiswahili hakijapewa nafasi sawa na Kiingereza katika utekelezaji wa sera ya lugha shuleni humo.

Kutokana na matokeo haya ni dhahiri kwamba sera ya lugha katika shule ya wasichana ya Itigo imependelea matumizi ya Kiingereza kama lugha ya mawasiliano baina ya wanafunzi.

***Umilikaji wa Biblia ya Kiswahili***

Umiliki wa biblia miongoni mwa wanafunzi ulichunguzwa ili kufahamu iwapo wanatumia biblia zilizoandikwa kwa lugha ya Kiingereza, Kiswahili au lugha nyinginezo. Matokeo yanaonyeshwa katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali 2: Umilikaji wa biblia miongoni mwa wanafunzi**

| Biblia | Idadi ya majibu | Asilimia % |
|---|---|---|
| Ya Kiswahili | 9 | 30% |
| Ya Kiingereza | 20 | 66.67% |
| Zote mbili | 1 | 3.33% |
| **Jumla** | **30** | **100%** |

Kutokana na matokeo katika *Jedwali 2* asilimia 30 (N=30) ya wanafunzi 30 waliohojiwa ilikiri kuwa wanamiliki bibilia iliyoandikwa kwa lugha ya Kiswahili. Sababu kuu ya kumiliki bibilia ya Kiswahili ni kuwa hueleweka kwa haraka mtu anapoisoma. Nayo asilimia 66.67 (N=20) ilithibitisha kuwa wanamiliki bibilia ya lugha ya Kiingereza. Sababu iliyotolewa na wanafunzi wanaomiliki bibilia ya Kiingereza ni kwamba lugha ya Kiingereza hutumika katika kufundisha somo la dini kwa hivyo biblia ya Kiingereza ni nyenzo muhimu katika kurahisisha uelewekaji wa somo la dini. Vile vile wanafunzi hawa walikiri kuwa ni sheria ya shule kwamba kila mwanafunzi anapojiunga na shule ya Itigo katika kidato cha kwanza, sharti aje na bibilia ya Kiingereza.

***Maoni ya Wanafunzi Kuhusu Katumizi ya Kiswahili na Kasisi wa Shule Anapohubiri***

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1422

Utafiti ulilenga kubaini ni kwa asilimia gani kasisi wa shule hutumia Kiswahili katika mahubiri yake. Matokeo yanaonyeshwa katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali 3: Maoni ya wanafunzi kuhusu matumizi ya Kiswahili na kasisi wa shule**

| Asilimia% | Idadi ya majibu |
|---|---|
| 25% | 18 |
| 50% | 12 |
| 100% | 0 |

Kutokana na matokeo katika *jedwali 3*, wanafunzi 18 kati ya 30 waliohojiwa walikiri kwamba wakati wa mahubiri kasisi wa shule hutumia Kiswahili kwa asilimia 25 wakati wa mahubiri. Nao wanafunzi 12 walikubali kuwa kasisi wa shule hutumia Kiswahili kwa asilimia 50 wakati wa mahubiri yake. Matokeo haya yanathibitisha kuwa Kiswahili kinatumika kwa viwango vya chini katika kuwasilisha ujumbe wa kidini kwa wanafunzi

### *Athari ya Matumizi ya Kiswahili katika Mahubiri*

Utafiti ulinuia pia kubaini kama matumizi ya Kiswahili katika mahubiri shuleni yana athari yoyote katika upokeaji na uelewekaji wa ujumbe uliokusudiwa. Matokeo kuhusiaa na swala hilo yanaonyeshwa katika jedwali lifuatalo

**Jedwali 4: Athari ya matumizi ya Kiswahili katika mahubiri**

| Athari | Idadi ya majibu | Asilimia% |
|---|---|---|
| Mahubiri yanaeleweka zaidi | 20 | 66.67% |
| Mahubiri hayeleweki vyema | 3 | 10% |
| Mhubiri haelewi lugha ya Kiswahili vyema | 1 | 3.33% |
| Hakuna athari yoyote | 6 | 20% |
| **Jumla** | **30** | **100%** |

Kutokana na matokeo katika *Jedwali 4* asilimia 66.67 (N=20) kati ya wanafunzi 30 waliohojiwa ilidai kuwa mhubiri anapotumia Kiswahili katika mahubiri yake ujumbe hueleweka zaidi na kwa haraka. Hii ina maana kwamba lugha ya Kiswahili inaeleweka zaidi miongoni mwa wanafunzi wa Itigo. Maoni haya yanawiana na maelekezo ya nadharia ya umilisi mawasiliano ya Dell Hymes (1966) kwamba lugha inayoeleweka na watu wengi ni nyenzo muhimu katika kufanikisha mawasiliano. Wakati huo huo, asilimia 10 (N=3) ilikiri kwamba Kiswahili kinapotumika katika mahubiri, mahubiri hayo hayaeleweki vyema. Kutokana na maoni katika hojaji, wanafunzi hawa walidai kwamba Kiswahili kina msamiati mgumu ambao huwatatiza na hivyo kuwa kizingiti katika uelewekaji wa mahubiri. Nayo asilimia 3.33 (N=1) walihoji kuwa mhubiri haelewi lugha ya Kiswahili vyema, hivyo hutatiza uelewekaji wa ujumbe wake wa kidini kwa wanafunzi. Hatimaye, asilimia 20 (N=6) ilidai kuwa hakuna athari yoyote Kiswahili kinapotumika katika mahubiri. Asilimia hii hupokea ujumbe vyema Kiswahili au Kiingereza kinapotumika. Kwao, lugha inayotumika si hoja. Wao hupokea ujumbe Kiswahili au Kiingereza kinapotumika kwa njia sawa.

## Uongozi na Mawasiliano ya Kidini Miongoni mwa Viongozi wa Wanafunzi

Katika sehemu hii, matokeo kuhusu matumizi ya Kiswahili miongoni mwa viongozi wa wanafunzi yanawasilishwa.

### *Matumizi ya Kiswahili katika Mikutano ya Viongozi wa Kidini wa Wanafunzi*

Utafiti ulilenga kubaini lugha inayotumika mara kwa mara katika mikutano ya viongozi wa kidini wa wanafunzi wa shule ya wasichana ya Itigo. Kutokana na matokeo katika jedwali 1.5, asilimia 70 (N=7) ya viongozi kumi waliohojiwa ilikiri kwamba wao

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

hutumia Kiswahili katika kuwasilisha hoja zao katika mikutano yao ya kupanga mikakati ya masuala ya kidini shuleni. Sababu yao kuu ni kwamba wana umilisi katika kuwasiliana kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Jambo hili huwapa ujasiri wa kutumia Kiswahili kuwasiliana. Sababu hii inashabihiana na maoni ya Dell Hymes (1966) katika nadharia ya umilisi mawasiliano kwamba jukumu kuu la matumizi ya lugha ni mawasiliano yanayofaa katika muktadha maalum. Nayo asilimia 30 (N=3) ilikiri kwamba wao hutumia lugha ya Kiingereza katika kuwasilisha maoni yao katika mikutano. Sababu kuu ya wao kutumia Kiingereza ni kwamba wanafunzi hawa wanashindwa kuzingatia kanuni za kisarufi katika kutumia Kiswahili. Kwa hivyo wao huona kuwa Kiingereza ni afadhali. Hata hivyo, Dell Hymes (1966) anapendekeza kwamba si lazima kuzingatia kanuni za kisarufi kwa kuwa lengo kuu la matumizi ya lugha ni kufanikisha mawasiliano. Anashikilia kuwa kanuni za kisarufi na mbinu nyinginezo zinatumiwa inapoonekana kuwa ni lazima.

**Jedwali 5: Matumizi ya Kiswahili katika mikutano ya viongozi wa kidini wa wanafunzi**

| Lugha | Idadi ya majibu | Asilimia% |
|---|---|---|
| Kiswahili | 7 | 70% |
| Kingereza | 3 | 30% |
| **Jumla** | **10** | **100%** |

***Lugha Inayotumika katika Uandishi wa Kumbukumba za Mikutano ya Viongozi wa Wanafunzi***

Eneo jingine liliozingatiwa katika utafiti huu lilikuwa kubaini lugha inayotumiwa na viongozi wanafunzi katika kuandika kumbukumbu za mikutano yao ya kidini. Matokeo yanaonyeshwa katika *jedwali 6.* Asilimia 10 (N=1) ya viongozi 10 waliohojiwa ilikiri kutumia Kiswahili katika kuandika kumbukumbu za mikutano yao ya kidini. Nayo asilimia 90 (N=9) walithibitisha kuwa wanatumia Kiingereza katika kuandika kumbukumbu wanapojadiliana kuhusu masuala ya kidini shuleni. Kutokana na matokeo haya ni wazi kwamba lugha ya Kiswahili inatumiwa kwa viwango vya chini mno katika uandishi wa kumbukumbu katika mikutano ya viongozi wanafunzi.

**Jedwali 6: lugha inayotumika kuandika kumbukumbu**

| Lugha | Idadi ya majibu | Asilimia% |
|---|---|---|
| Kiswahili | 1 | 10% |
| Kingereza | 9 | 90% |
| **Jumla** | **10** | **100%** |

**Maoni ya Kasisi wa Shule Kuhusu Uongozi Na Mawasiliano Ya Kidini Shuleni**

Utafiti ulilenga kupata maoni ya kasisi wa shule kuhusu masuala ya uongozi na mawasiliano ya kidini katika shule ya wasichana ya Itigo. Matokeo yanawasilishwa ifuatavyo;

***Biblia Zinazotumiwa Na Kasisi Wa Shule***

Kutokana na majibu katika hojaji ya kasisi wa shule ilibainika kuwa kasisi wa shule anamiliki biblia ya Kiingereza na biblia ya Kiswahili. Majibu zaidi yalionyesha kuwa kasisi wa shule hutumia biblia hizi kwa viwango sawa. Ilidhihirika kuwa biblia ya Kiswahili hutumika kupata ufafanuzi zaidi. Maoni ya kasisi wa shule ni kuwa Kiswahili hueleweka zaidi na hivyo humsaidia katika kuandaa mahubiri yake. Jambo hili ni muhimu sana katika kukuza na kuendeleza matumizi ya lugha ya Kiswahili. Matumizi ya biblia ya Kiswahili kupata ufafanuzi zaidi humwezesha kasisi wa shule kuwasilisha maudhui ya kidini kwa urahisi. Kwa hivyo hufanikisha mawasiliano kama anavyohoji Dell Hymes (1996) katika nadharia ya umilisi mawasiliano.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1422

***Lugha Inayotumiwa Na Kasisi Wa Shule Katika Mahubiri.***

Utafiti ulilenga kubaini lugha inayotumika mara nyingi katika mahubiri shuleni. Kwa hivyo kasisi wa shule alihusishwa katika ujazaji wa hojaji ili kupata data kuhusu matumizi haya ya lugha. Vile vile uchunzaji wa ibada za Jumapili ulifanywa kwa lengo la kufahamu lugha inayotumika. Kutokana na majibu katika hojaji na uchunzaji wa ibada za Jumapili ilibainika kuwa kasisi wa shule hupendelea kutumia Kiingereza katika mahubiri yake. Sababu kuu ya kukosa kutumia Kiswahili ni kwamba Kiswahili kinahitaji uzingatiaji wa sheria za kisarufi. Kasisi alikiri kukosa umilisi wa kanuni za sarufi ya Kiswahili. Hata hivyo kasisi hakupaswa kutishiwa na uzingatiaji wa sarufi kwani Dell Hymes (1966) anapendekeza kwamba vipashio muhimu vya lugha si vile vya kisarufi na kimuundo tu bali pia vile vya kimawasiliano. Kwa hivyo uwasilishaji bora wa ujumbe wa kidini ni muhimu zaidi.

**HITIMISHO**

Utafiti huu uliluhusu matumizi ya Kiswahili katika uongozi na mawasiliano ya kidini katika shule ya wasichana ya Itigo. Utafiti ulilenga kubaini jinsi lugha ya Kiswahili inavyotumika katika kufanikisha masuala ya kidini. Vilevile, ulilenga kuchunguza sera ya matumizi ya lugha katika shule ya wasichana ya Itigo. Viongozi wa kidini wa wanafunzi vile vile walihojiwa kwa lengo la kufahamu jinsi ambavyo wanatumia lugha katika mikutano yao na katika kuwasilisha maudhui ya kidini. Kasisi wa shule ni muhimu sana katika kuwakuza wanafunzi katika masuala ya kiroho. Kwa hivyo alihusishwa katika utafiti kwa lengo la kubaini jinsi ambavyo anatumia lugha ya Kiswahili. Isitoshe, ibada za Jumapili zilihudhuriwa kwa lengo la kupata data zaidi.

Matokeo ya utafiti yalithibitisha kuwa sera ya lugha katika shule ya wasichana ya Itigo haijaipa lugha ya Kiswahili nafasi muhimu na badala yake hupendelea matumizi ya lugha ya Kiingereza. Ilibainika vilevile kuwa wanafunzi wengi wanamiliki bibilia za Kiingereza. Wachache tu ndio wanamiliki bibilia za Kiswahili. Sababu kuu ni kuwa lugha ya Kiingereza inatumika katika kufundisha somo la dini. Kwa hivyo bibilia ya Kiingereza ni muhimu katika kukuza somo la dini. Matokeo ya maoni ya wanafunzi yalithibitisha kuwa kasisi wa shule hupendelea Kiingereza katika mahubiri yake. Ilibainika pia kuwa Kiswahili kinatumika kwa asilimia 25% tu katika mahubiri.

Matokeo ya utafiti yalithibitisha pia kuwa asilimia kubwa ya viongozi wanafunzi (90%) hutumia Kiswahili katika kuwasilisha maudhui yao ya kidini. Hata hivyo ilibainika kuwa lugha inayotumiwa mara nyngi na viongozi hawa katika uandishi wa kumbukumbu za mikutano yao ni Kiingereza. Japo Kiswahili kinatumika katika majadiliano yao, Kiingereza kinatumika katika kuandika kumbukumbu za majadiliano haya.

Ilibainika vile vile kuwa kasisi wa shule hutumia bibilia ya Kiswahili na ya Kiingereza. Matokeo ya utafiti yaliweka wazi kuwa bibilia ya Kiswahili hutumika katika kupata ufafanuzi zaidi. Kutokana na majibu ya hojaji na matokeo ya uchunzaji, ilibainika kuwa lugha ya Kiingereza hutumika zaidi katika mahubiri huku Kiswahili kikitumiwa kwa kiwango cha chini sana. Inapendekezwa kuwa utawala wa shule ya Itigo uchunguze upya sera ya lugha shuleni. Matumizi zaidi ya Kiswahili yatakuwa na manufaa kwani ni bayana kuwa lugha hiyo inafanikisha mawasiliano ya kidini zaidi ikilinganishwa na Kiingereza.

**MAREJELEO**

Davis, S.C (1976). Basic Principals of Functional Grammar in Syntax and Semantics, Volume 13. New York: Academic Press

Hymes, D. (1972). Models for the interaction of language and social life. In J. J. Gumperz & D.H. Hymes (Eds.), Directions in sociolinguistics: The ethnography of communication (pp. 35–71). New York: Holt, Rinehart and Winston.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1422

Kipchirchir, M. (2019). Matumizi ya Vifaa vya Kisasa katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Sarufi katika shule za Upili zilizoko kaunti ndogo ya Moiben, Uasin Gishu. Tasnifu ya Uzamili. Chuo kikuu cha Kibabii.

Kothari, C (1993). Research Methodology, Methods, and Techniques. New Delhi: Wiley Eastern Limited.

Massamba na Wenzake (2001). Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu. Dar es Salaam: TUKI.

Misiko, D (2008). Matumizi ya Kiswahili katika Mawasiliano Rasmi Nchini Kenya: Uchunguzi kifani wa Wilaya ya Uasin Gishu. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Moi.

Mugenda, O., & Mugenda, A. (2003). Research Methods, Qualitative & Quantitive Approaches. Nairobi: ACTS Press.

Musau, M (2001). The Spread of Kiswahili in Kenya in the New Millenium: Prospects and Challenges. Dar es Salaam: TUKI.

Mbaabu, I (1978). Kiswahili Lugha ya Taifa. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Oduori, R (2002). Dhima ya Kiswahili katika Maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Eldoret: Moi University Press.

Osore, K (2002). The Role of Language in Scientific and Technological Development: The case of Kiswahili Language in East Africa. Hammanskraal University: Pretoria.

Onen, D. (2005). A General Guide to Research Proposal and Report. Oxford: Oxford University Press.

Sharman, D. (1983). Research Methods in Social Science. New Delhi: Sterling Publishers.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.